

HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

SHULE YA SEKONDARI USHIRIKA

SIMU (MKUUWA SHILE): 0713-342619/0625-763493
SIMU (MTAALUMA): 0623-023948

S.L.P 322
NEWALA

TAREHE.....

KUMBU NA.

MZAZI/ MLEZI (Isomwe mbele ya mwanao)

.....

AF Na.....

YAH: TAARIFA YA MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI

1. PONGEZI

Nafurahi kukuarifu kwamba mtoto wako (mtajwa hapo juu) amechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari, kidato cha kwanza mwaka 2021. Namsihi kijana huyu kuhakikisha kuwa hapotezi nafasi yake.

2. UKARIBISHO

Kwa niaba ya jumuiya ya Ushirika Sekondari, napenda nimkaribishe motto wako katika shule yetu ambayo ni taasisi kamili ya kitaaluma. Ni matumaini yangu kuwa mtoto atayapokea na kuyamudu maisha mapya ya kitaaluma kwa muda wake wote wa kuwa hapa shuleni (usiopungua miaka minne)

3. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Ushirika ipo Halmashauri ya wilaya ya Newala kati ya vijiji vya Magombo na Mkwedu. Shule yetu imekatizwa na barabara itokayo Newala mjini kuelekea Mtunguru. Aidha hii imebahatika kwa kuweza kufikika kirahisi kutokea upande wowote wilayani hapa.

4. KICHOKOO

Kichokoo cha shule (School Motto) ni tamko rasmi la kutoa Mwelekeo wa shule. **KICHOKOO** cha shule ni **"DISCIPLINE BRINGS SUCCESS"** yaani **"NIDHAMU HULETA MAFANIKIO"**. Akiwa hapa shuleni tunamtarajia mwanao aishi kukabiliana na MOTTO wa shule.

5. MAANDALIZI

Mara tu upatapo barua hii jitahidi kumwandaa mwanao kwa kufanya yafuatayo;-

- Kumtafutia mahitaji yote ya shule
- Kumpeleka kituo cha afya au hospitali kupima afya

- Kwa asiye na cheti cha kuzaliwa aende mahakamani kwa ajili ya kupata “*Affidavit*” ili kukamilisha ujazwaji wa fomu zilizoambatanishwa katika barua hii. (inashauriwa zaidi apelekwe kituo cha afya Mkwedu ambacho kipo ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Newala)

6. A. **SARE RASMI YA DARASANI** (Anunue mzazi mwenyewe)

➤ **WASICHANA**

- Sketi mbili (2) za rangi ya khaki (kitambaa cha suti namba 1). Urefu wake uvuke magoti na iwe na marinda. **WAVEZA KUANGALIA SAMPULI HAPA SHULENI**
- Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi (*Tomato*)
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi 2. (vya kike)
- Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi
- Vazi la hijabu (kwa anaependa) lifike kitovuni
- Sweta la bluu.

➤ **WAVULANA**

- Suruali mbili (2) rangi ya Khaki (kitambaa cha suti NAMBA 1)
- **Suruali isiwe ya kubana, PINDO LA CHINI LAZIMA LIWE INCHI SABA. (MZUNGUKO WOTE INCHI 14)**
- Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi
- Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi
- Soksi za khaki jozi mbili (2)
- Sweta la bluu

B. **SARE ZA MICHEZO NA KAZI ZA NJE** (Anunue mzazi)

➤ **WASICHANA**

- Gauni la kijani
- Tracksuit rangi ya **Dark Blue au Blue**
- Soksi za khaki
- Viatu vya raba
- Tisheti ya shule rangi ya **dark blue** (Zinapatikana shuleni)

C. **VIFAA VYA DARASANI**

- Daftari kubwa 10 kubwa na Counter Books chache kwa mwenye uwezo
- Mkebe wa hisabati
- Rula ndefu ya sentimita 30 nyeupe
- Kalamu za kutosha
- Dictionary (English- Kiswahili). **NI MUHIMU SANA**

ZINGATIA: KILA MTOTO ANATAKIWA AJE NA VITU VIFUATAVYO

✚ KIASI CHA **SH. 5000 (ELFU TANO)** KWA AJILI YA KUPATA BIMA YA AFYA (**CHF- ILIYOBORESHWA**)

- ✚ NDOO MOJA NDOGO
- ✚ REAM 1 (A4) (BUNDA LA KARATASI)
- ✚ SPRING FILE 1
- ✚ PICHA (PASSPORT SIZE 4)
- ✚ JEMBE NA FYEKEO (WASICHANA)
- ✚ JEMBE NA PANGA (WAVULANA)

7. MAELEKEZO MENGINEYO

- Shule itafunguliwa/ imefunguliwa tarehe 11/01/2021
- Kidato cha kwanza wataripoti tarehe 11/01/2021
- Ni muhimu siku hiyo umlete wewe mzazi ili upate maelekezo ya ziada katika SEMINA maalumu ya wazazi itakayofanyika kuanzia saa 3:00 asubuhi
- Siku ya semina kutakuwepo na mengi yakiwemo
 - I. Kusomewa kanuni na taratibu za kumhudumia mtoto kwa kipindi chote cha masomo yake
 - II. Kuwasilisha fomu za ukaguzi wa afya ya mwanao. Ukaguzi huo usifanyike katika zahanati yoyote isipokuwa pale ulipoelekezwa tu.
 - III. Kuwasilisha kivuli cha cheti cha kuzaliwa "Birth Certificate"
 - IV. Kurejesha fomu za ahadi/Mkataba (ikiwa imejazwa)
- Hakikisha mzazi unahudhuria semina hiyo
- Taarifa ya ugonjwa wa mwanafunzi (kwa miaka yote) italetwa na mzazi/ mlezi na SIO kumtuma mwanafunzi mwenzake
- Shule inatoa chakula cha mchana kupitia utaratibu wa uchangiaji waliojiwekea wazazi wenyewe. Utapewa maelekezo na utaratibu mzima siku ya semina.
- Usichelewe kumleta mwanao bila sababu za msingi na kwa kufanya hivyo unaweza kumpotezea nafasi mtoto wako. Mtoto anaweza kuanza masomo hata kama hajakamilisha vifaa vyote (ZIKIWEMO SARE ZA SHULE)

KILA KHERI NA KARIBU USHIRIKA TUSHIRIKIANE KATIKA ELIMU

.....
 NANDONDE E.L
 MKUU WA SHULE

Nakala: Afisa Elimu Sekondari
 Halmashauri ya Wilaya
 S.L.P 16
 NEWALA